**TAARIFA YA UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA NA USTAWI WA JAMII KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA WAZEE DUNIANI**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA**

**TAREHE: 01 OCTOBA, 2017**

**Mheshimiwa Mgeni rasmi,** Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Sophia Mjema,

Mganga Mkuu wa Mkoa, Dr.Grace Magembe
Afisa Tarafa wa Wilaya ya Ilala,
Mhe.Naibu Meya wa Manispaa ya Ilala,

Ndugu Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala,

Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa ya Ilala,

Viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa

Wataalamu mbalimbali mliopo ngazi ya Mkoa na Wilaya,

Watendaji wa Kata za Manispaa ya Ilala,

Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wa Manispaa ya Ilala,

Viongozi wa Asasi zisizo kuwa za Kiserikali,

Wazee kutoka kata mbalimbali mliopo hapa,
Wageni Waalikwa,
Waandidhi wa habari,
Mabibi na Mabwana.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema, na kutuwezesha kufika hapa tukiwa na afya njema. Aidha nichukue fursa hii kukukaribisha wewe na wageni wote waalikwa katika Manispaa ya Ilala katika siku hii adhimu na ya kipekee katika Siku ya Wazee Duniani. Siku ambayo kwetu sisi ni siku ya kujivunia kwa kutuwezesha uzinduzi wa vitambulisho vya Msamaha kwa wazee wote waliopo katika Manispaa yetu.
Pia tunapenda kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamiii, Jinsia, Wazee na Watoto ambayo ndio imebeba dhamana kubwa ya kuhakikisha Afya za wananchi zinaboreshwa kwa kupatia sera na miongozo ya utoaji wa huduma bora za tiba na kinga kwa makundi yote ya kijamii.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ina jumla ya wakazi wapatao 1,528,489 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012. Huduma za afya zimeendelea kutolewa kwa wananchi hawa katika vituo vya tiba **29** ikiwa ni pamoja na Hospitalini 2, vituo vya Afya 3, Zahanati 23 na kliniki moja ya magonjwa yanayoambukiza(IDC). Aidha Vituo vyote hivi vinatoa huduma ya Afya kwa wazee wasiojiweza kwa mfumo wa Msamaha ambao kwa mwaka 2016/2017 jumla ya wagonjwa 193,557 walipatiwa matibabu kwa msamaha ambayo yaligharimu kiasi cha shilingi **1,151,998,310/=** . Katika kipindi hiki jumla ya wazee 17,589 walipatiwa huduma mbalimbali za msamaha katika vituo vya kutolea huduma za afya.

***Mheshimiwa Mgeni rasmi;***

Kauli mbiu ya mwaka huu ni "**Kuelekea Uchumi wa Viwanda, Tuthamini Mchango, Uzoefu na Ushiriki wa Wazee kwa Maendeleo ya Taifa**". Maadhimisho haya ya siku ya Wazee Duniani katika Halmashauri Manispaa ya Ilala yenye yanaambatana na utoaji wa Vitambulisho vya Wazee kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya na huduma nyingine za kijamii. Hii ni katika utekelezaji wa sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 kwa lengo la kuhakikisha kuwa wazee wa Tanzania wanatambuliwa na kupewa fursa ya kushiriki katika mambo yanayohusu maisha yao ya kila siku kwa manufaa yao na kwa manufaa ya watanzania wote.

Kwa mujibu wa taarifa za MTUHA za mwaka 2016 inaonyesha kuwa; Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ina jumla ya wazee wapatao **44,222** kutoka katika kata 36 zilizopo. Hadi sasa tunaendelea na usajili na tayari Wazee **15,000** wasiojiweza wameshapigwa picha tayari kwa kuvirudufu na kuwapatia vitambulisho hivyo. Leo hii utawapatia wawakilishi wao vitambulisho hivi vikiwa tayari kwa matumizi. Aidha zoezi hili ni endelevu; lengo likiwa kuwafikia wazee wote ifikapo Juni 2018.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Tunatoa wito kwa wazee wote walioko Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kuendelea kujitokeza kwa wingi kwenye Kata zao na kujiandikisha ilikupata vitambulisho vya Msamaha ili waweze kupata huduma za Afya katika vituo vyetu vya kutolea huduma. Vitambulisho hivi ni muhimu ili

kumtambua mzee anayestahili kupata huduma za afya na huduma zinginezo na kumuondolea usumbufu wakutafuta barua kutoka Serikali za Mtaa.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Tuna changamoto mbalimbali katika uendeshaji wa huduma za afya na hasa katika kuwahudumia wazee hawa. Gharama za uendeshaji wa huduma za msamaha zimekuwa ni kubwa katika vituo vya kutolea huduma za afya. Hii ni kutokana na idadi kubwa ya wagonjwa wanaohitaji msamaha, wakiwemo akina mama wajawazito, watoto chini ya miaka mitano, walemavu na wazee. Wazee pia wana changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na magonjwa.Magonjwa ambayo yanaripotiwa kwa wazee katika vituo vyetu vya kutolea huduma ni pamoja na Magonjwa ya Moyo, Shinikizo la juu la damu (presha), Kisukari, saratani ya tezi dume, saratani ya shingo ya kizazi , saratani ya matiti, Magonjwa ya Macho, Homa ya mapafu na Magonjwa yatokanayo na uzee (mifupa, mgongo). Aidha tuna upungufu mkubwa watumishi katika vituo vyote na hasa kwa upande wa kada ya wauguzi.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi;***

Pamoja na changamoto hizo zinazoikabili Halmashauri yetu ya Manispaa ya Ilala; Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imeweka mikakati mbalimbali ya kutatua changamoto hizo:-

1. Kwa mwaka huu wa fedha **2017/2018** zaidi ya **33.3%** ya ukomo wa bajeti tuliyopewa imetengwa kwa ajili ya kununua dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Aidha tunaomba kuongezewa mgao wa ruzuku ya dawa kutoka Serikali kuu kwa ajili ya Hospitali ya Mama na Mtoto iliyopo Chanika iliyojengwa kwa ufadhili wa watu wa Korea Kusini; ilikuweza kukabiliana na wingi wa wagonjwa tunao wahudumia.

2. Tumeomba katika ikama ya mwaka 2017/18 watumishi **208** ambapo watakapoajiriwa tutakuwa tumepunguza uhitaji huu kwa kiwango kikubwa.

***Mheshimiwa mgeni Rasmi;***

Mwisho napenda nitoe shukrani za dhati kwako wewe binafsi kwa kukubali kuja kuwa mgeni rasmi katika siku hii muhimu kwa wazee wetu. Aidha ninawashukuru wadau wote waliochangia na wanaoendeleo kuchangia shughuli za afya na ambao wameshiriki hapa hasa HELPAGE

International. Wadau hawa wameendeleea kuboresha huduma zetu katika maeneo mbalimbali.

Tunakutakia Afya njema katika kutekeleza majukumu yako kwa wananchi wa  Wilaya ya Ilala na watanzania.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza;

Dr. Victorina Ludovick

Mganga Mkuu wa Manispaa

**Halmashauri ya Manispaa ya Ilala**